**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUPOKEA KOMBE LA UBINGWA WA AFRIKA MASHARIKI NA KATI (*CECAFA*)KWA VIJANA WENYE UMRI YA CHINI YA MIAKA 23 NA KUWAPONGEZA WASHIRIKI WA MASHINDANO YA OLIMPIKI MWAKA 2021**
**IKULU, DAR ES SALAAM, TAREHE 21 AGOSTI, 2021**

***Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;***

***Mheshimiwa Pauline Gekul, Naibu Waziri wa Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo;***

***Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii;***

***Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu, Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo;***

*Bi. Neema Msita, Kaimu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT);*

*Viongozi wengine wa Serikali mliopo;*

*Viongozi wa Vyama na Mashirikisho ya Michezo nchini (TFF, Bodi ya Ligi, Kamati ya Olimpiki na Shirikisho la Riadha);*

*Wachezaji wetu wa Timu ya Taifa Chini ya Miaka 23;*

*Wana-Riadha wetu mlioshiriki Michezo ya Olimpiki;*

*Ndugu Wana-Habari, Mabibi na Mabwana:*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## SALAMU

- Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kukutana hapa. Tumekutana hapa, kwanza, ili kuipongeza Timu yetu ya Taifa ya Chini ya Umri wa Miaka 23 kwa kuchukua Ubingwa wa Mashindano ya Afrika Mashariki na Kati pamoja na wana-riadha wetu walioshiriki Mashindano ya Olimpiki hivi karibuni.

- Hii sio mara yangu ya kwanza kukutana na Timu ya Taifa. Nakumbuka, mwaka 2017, wakati nikiwa Makamu wa Rais, nilipokea Kombe la Ubingwa wa Afrika Mashariki kwa Timu ya Vijana chini ya Miaka 17, *Serengeti Boy*s. Kwa hiyo, hii ni mara ya pili

kukutana na Timu zetu za Taifa zilizofanya vizuri ili kuwapongeza. Lakini, niseme tu, mbali na kuzipongeza, tumekutana hapa ili kuzipa hamasa Timu zetu za Taifa za michezo mbalimbali kufanya vizuri zaidi kwenye mashindano ya kimataifa na kulitangaza vyema jina la nchi yetu.

**RAMBIRAMBI**

- Kabla sijaendelea zaidi, napenda kutumia fursa hii kutoa pole nyingi kwa familia ya mpira wa miguu Tanzania kwa kuondokewa na wadau wenu. Kwanza, aliyekuwa Mwenyekiti wa BMT na pia FAT, hivi sasa TFF, Marehemu Mzee Said El Maamry; na pili Mchambuzi wa Michezo Mashuhuri na Mtangazaji wa Mpira wa TBC, Marehemu Alex Kashasha.

- Naomba tusimame kwa dakika moja tuwakumbuke. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho zao mahali pema peponi. **Amina.**

**UMUHIMU WA MICHEZO**

- Michezo ni sekta kubwa ambayo inaendelea kukua kwa kasi ulimwenguni. Kwa mujibu wa Jarida la *Forbes*, sekta hii inakadiriwa kuwa na thamani ya **Dola za Marekani trilioni 1.3** na kutoa ajira nyingi za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

- Vilevile, michezo inasaidia kutangaza nchi. Wapo watu wengi duniani waliifahamu nchi yetu kwenye miaka ya 1970 na 1980 kupitia wana-Riadha wetu maarufu, Filbert Bayi, Selemani Nyambui na Juma Ikangaa; na nafahamu wengine wameifahamu nchi yetu kupitia

Wanariadha wetu, Alphonce Simbu pamoja na *mwanangu* Failuna Abdi ambao walituwakilisha kwenye Olimpiki ya Tokyo; na wengine kupitia Timu zetu za Taifa, hususan za Vijana na Wanawake, ambazo zimefanikiwa kuchukua Makombe mbalimbali.

- Kwa upande mwingine, wapo Watanzania wengi wameifahamu Argentina kupitia Maradona na Messi; Brazil kupitia Pele, Ronaldo na Ronadinho; Ethiopia kupitia Gebre Selassie, Liberia kupitia George Weah, Philipinnes kupitia Manny Pacquiao; Jamaica kupitia Usain Bolt. Hii inaonesha umuhimu wa michezo katika kuitangaza nchi.

- Zaidi ya hapo, kama sote tujuavyo, michezo inaburudisha, inajenga urafiki na halikadhalika mshikamano kwenye Taifa. Sambamba na hayo, michezo ni afya. Mathalan, hivi sasa dunia inakabiliwa na ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukiza (moyo, figo, kisukari, saratani au kansa, n.k.), ambapo mwaka 2016 yalisababisha **asilimia 71** ya vifo. Kwa hapa nchini, takwimu zinaonesha kwamba, mwaka 2017, magonjwa yasiyoambukiza yalisababisha **asilimia 33** ya vifo. Ili kupunguza magonjwa haya, wataalamu wanatushauri kushiriki kwenye michezo au kufanya mazoezi. Tunatakiwa kufanya mazoezi kwa angalau nusu saa kwa siku mara tatu kwa wiki.

## PONGEZI

***Waheshimiwa Viongozi na Wanamichezo mliopo;***

- Kama mnavyofahamu, wakati nikilihutubia Bunge tarehe 22 Aprili, 2021 niliahidi kwamba Serikali ya Awamu ya Sita itaendeleza juhudi za kuboresha na kukuza sekta ya michezo nchini. Ni kwa msingi huo, leo nimefurahi sana kuwepo mahali hapa kupokea Kombe hili la Ubingwa wa Afrika Mashariki kwa Vijana wenye Umri Chini ya Miaka 23. *"Kila safari huanza na hatua moja"*.

- Hivyo basi, nawapongeza sana vijana wetu kwa kutuletea kombe hili. Ni imani yangu kuwa, ushindi huu utaleta hamasa kwa Timu zetu nyingine za Taifa

kucheza kwa bidii. Na katika hilo, natambua kuwa Timu zetu za Taifa za Mpira wa Miguu za Wanaume (*Taifa Stars*) na Wanawake (*Twiga Stars*) zipo kwenye maandalizi ya mashindano mbalimbali. *Taifa Stars* inajiandaa na Michezo ya Kufuzu kwa Mashindano ya Kombe la Dunia ya Mwaka 2026; na *wanangu* Twiga Stars wanajiandaa kushiriki Mashindano ya COSAFA nchini Afrika Kusini.

- Vilevile, Timu ya Vijana ya Mchezo wa Wavu inajiandaa kwa Mashindano ya Afrika; na halikadhalika, mwaka huu, mwezi Novemba, nchi yetu itakuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa watu wenye Ulemavu. Niwasihi sana viongozi wa michezo kuwaandaa na kuwalea vizuri vijana wetu ili

watuwakilishe vyema kwenye mashindano hayo na kuipeperusha vizuri Bendera yetu. Wachezaji wetu watapata hamasa na ari ya kucheza kwa kujituma endapo watatunzwa na kulelewa vizuri.

## MIPANGO YA SERIKALI KUKUZA MICHEZO

***Ndugu Viongozi wa Michezo;***
***Ndugu Wachezaji, Ndugu Wana-Habari,***
***Mabibi na Mabwana:***

- Serikali imedhamiria kwa dhati kabisa kukuza na kuendeleza sekta ya michezo nchini. Na katika hilo, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri anayehusika na masuala ya Michezo, tayari tumeanzisha Mfumko wa Maendeleo ya Michezo ili kusaidia Timu za Taifa. Kwa kuanzia, Mwaka huu wa Fedha, tumetenga **shilingi bilioni 1.3**; lakini tutaendelea kuutunisha Mfuko huo.

- Sambamba na hayo, tumeondoa VAT kwa ajili ya nyasi bandia ili kuwezesha viwanja vyetu kuboreshwa. Tutaendelea pia kuangalia maeneo ya vifaa vingine vya michezo, kama ilivyoombwa. Zaidi ya hapo, hivi sasa tunajenga Kituo cha Kulea Vipaji vya Michezo (*sports academy*) kwenye Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya (Mwanza), na tutaendelea kujenga maeneo mengine. Aidha, tumepanga kujenga viwanja vitatu vya mazoezi (Dar es Salaam, Dodoma na Geita).

- Vilevile, tumeanza kufanya tathmini ya kujenga Kituo cha Kisasa cha Michezo na Kazi za Sanaa za Ndani (*Arts and Sports Arena*), ambacho ni ombi la muda mrefu la wanamichezo nchini. Kituo hicho sio tu kitasaidia kuikuza michezo nchini bali pia kitaiwezesha

nchi yetu kuandaa michezo mikubwa ya kimataifa, hususan mpira wa pete, mpira wa wavu, mpira wa kikapu na bila kusahau ndondi. Tunakusudia kujenga vituo viwili; kimoja hapa Dar es Salaam, na kingine kule Dodoma; lakini kwa awamu.

- Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine kwa kurejesha upya hamasa ya michezo ya shule za msingi na sekondari na pia mipango yenu ya kufufua Mashindano ya Taifa itakayoshindiwa na mikoa kwenye michezo mbalimbali. Aidha, nawapongeza kwa kubuni wazo la kuanzisha Tamasha la Kila Mwaka (*Tanzanite Women Sports Festival*). Hatua hizi, naamini zitasaidia kukuza sekta ya michezo nchini.

- Lakini niseme, pamoja na jitihada hizi za kukuza michezo, kuna haja ya kuwaangalia kwa jicho la pekee wanawake, hususan wa mpira wa miguu. Leo tumejisifu hapa kwamba wameleta makombe manne; lakini sisi kama Taifa tujiulize tumewafanyia nini? Hivyo basi, nitoe rai kwamba, Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ulioanzishwa, uangalie maslahi au hatma ya baadaye ya wachezaji wetu, hususan wa Timu za Taifa za Wanawake ili wasihangaike sana baada ya kustaafu. Nakumbuka, Timu yetu ya Taifa ilipofuzu kushiriki Mashindano ya Kombe la Afrika, tuliwapatia wachezaji viwanja kule Dodoma. Lakini, kwa Timu za Wanawake, licha ya kuleta makombe, hatujawahi kuwafanyia chochote. Hivyo, ni vyema tulitafakari

suala hili. Sisemi hivyo kwa kuwatetea wanawake bali kwa kutetea haki.

**WITO**

- Kabla ya kuhitimisha, naomba nitoe wito kwa Wizara, Mashirikisho na Vyama vya Michezo, Vilabu pamoja na wanamichezo wenyewe, kujipanga vizuri. Na hapa nina maneno kidogo kuhusu Kamati ya Olimpiki. Mwanzoni mwa hotuba yangu nimewapongeza wanariadha wetu watatu walioshiriki Mashindano ya Olimpiki nchini Japan hivi karibuni. Hata hivyo, ukweli ni kwamba, kwa Taifa kubwa kama letu, kuwakilishwa na wachezaji watatu tena wa mchezo mmoja ni aibu.

- Hivyo basi, natoa changamoto kwenu kujifanyia tathmini ili kwenye Mashindano yajayo yatakayofanyika Paris mwaka 2024 ushiriki wetu uwe mkubwa kwa idadi ya wanamichezo na sio viongozi; lakini pia tupate ushindi. Tanzania ina wanamichezo wengi, hivyo, tujipange vizuri, ikiwemo kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali (majeshi, mikoa) tunaweza kupata wachezaji wengi wazuri watakaotuwakilisha na kutuletea ushindi. Hiyo ndiyo changamoto ninayoitoa kwa Kamati ya Olimpiki pamoja na viongozi wa michezo mingine.

- Sambamba na hilo, napenda kuungana na Mheshimiwa Waziri wa Michezo katika kuhimiza utawala bora kwenye sekta ya michezo. Jitihada zetu kukuza

michezo hazitafanikiwa endapo suala la utawala bora halitapewa kipaumbele kwenye Vyama, Mashirikisho na Vilabu vya Michezo. Hivyo, nawahimiza kuimarisha utawala bora kwenye michezo. Mkifanya hivyo, mtatuhamasisha na sisi tuliopo Serikalini kushughulikia changamoto mliizotueleza.

- Na katika hilo, naiagiza BMT kulisimamia suala hili. Kwa bahati nzuri, Kaimu Katibu Mtendaji wa BMT ni mwanamke; na kama tujuavyo, wanawake wakipewa jambo hawashindwi. Hivyo, naamini utakwenda kutumia maarifa yako kulisimamia suala hili. Sambamba na hilo, natoa wito kwa wanamichezo kupata chanjo ya *Corona* ili kujilinda na ugonjwa huo lakini pia kuwawezesha kushiriki michezo nje ya nchi.

- Naihimiza pia sekta binafsi ya ndani na kutoka nje kuwekeza kwenye michezo hapa nchini. Kama nilivyosema awali, mchezo ni biashara kubwa duniani. Na hapa, naipongeza Kampuni ya AZAM kwa jinsi inavyojitahidi kuwekeza kwenye mchezo wa mpira wa miguu pamoja na ndondi (*wenyewe wanaita* ***vitasa***). Naziomba kampuni nyingine ziige mfano.

- Vilevile, natoa wito kwa vijana na pia wazazi kuwahimiza watoto wao kushiriki kwenye michezo. Kama nilivyosema, mbali na kwamba michezo ni ajira na biashara, michezo ni afya na pia michezo inasaidia kuwajenga watoto wetu kwenye maadili mema. Na kwa bahati nzuri michezo ipo mingi (mpira wa miguu,

pete, wavu, kikapu, riadha, mbio za baiskeli, kuogelea, *tennis*, kuruka juu, sarakasi, n.k.).

- *Mabibi na Mabwana;* mwakani kutafanyika Mashindano ya Kombe la Dunia nchini Qatar. Hapa na Qatar sio mbali, hivyo, naamini tukijipanga vizuri nasi tunaweza kunufaika na Mashindano hayo. Kwa hiyo, natoa wito kwa wadau wa sekta ya umma na binafsi kujipanga ili kutumia fursa hiyo. Wizara ya Utalii wanaweza kutengeneza *special packages* ili kuwavutia watakaokwenda kuangalia mashindano hayo kutembelea vivutio vyetu; na kwa Wizara ya Viwanda na Biashara na wafanyabiashara wanaweza kuangalia fursa ya kuuza bidhaa zetu nchini Qatar (nyama, samaki, korosho, mchele, matunda, n.k.)

## HITIMISHO

- Nihitimishe kwa kurudia kuwapongeza vijana wetu kwa kuchukua Kombe la CECAFA pamoja na wana-riadha wetu waliotuwakilisha kwenye Mashindano ya Olimpiki mwaka huu. Nimekuja na zawadi ndogo kwenu kwa ajili ya kuwapa hamasa zaidi. Aidha, nazihimiza Timu za michezo mingine zitakazoshiriki kwenye mashindano ya kimataifa, vikiwemo vilabu, kujiandaa vyema na kucheza kwa kujituma ili kupeperusha vyema bendera ya nchi yetu.

- Mwisho kabisa lakini sio kwa umuhimu, wakati tukiwa tumekaa pale mezani, Rais wa TFF, Bwana Wallace Karia, alinidokeza kuhusu ombi la Udhamini wa Mashindano ya Afrika Mashariki na Kati kwa Timu za

Taifa za Wanawake. Alinishawishi sana kwa kutoa mfano wa Mashindano ya *Kagame Cup*, nami baada ya kutafakari, nimeamua kukubali ombi hilo; ambapo nitatafuta baadhi ya watu nishirikiane nao.

- Baada ya kusema hayo.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**"Ahsanteni sana kwa Kunisikiliza"**